NIPASHE UK 15.

# Jafo awataka wafugaji kufuga kwa tija kuepuka uharibifu mazingira

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, amewataka wafugaji nchini kuhifadhi mazingira kwa kufanya shughuli za ufugaji wenye tija kwa maendeleo endelevu.

Dk. Jafo aliyasema hayo jana kwenye uzinduzi wa wiki ya maonesho ya ufugaji wenye tija na utunzaji wa mazingira sanjari na kuzindua Chama cha Mazingira na Ufugaji Tija Tanzania (CHAMAUTA), jijini hapa.

Alisema ufugaji endelevu usioathiri hifadhi ya mazingira utasaidia kuepusha migogoro baina ya wakulima na wafugaji nchini.

"Tuepuke migogoro baina ya wakulima na wafugaji ambayo tunashuhudia ikitokea katika baadhi ya mikoa nchini husababisha kutoelewana kwa makundi haya mawili hali inayoweza kusababisha uvunjifu wa amani, na tuna wajibu wa kulinda amani," alisisitiza.

Aidha, alihimiza wafugaji ambao wamepata ufadhili kutumia fursa ya mkutano wa 28 wa nchi wanachama wa Mkataba wa Mabdiliko ya Tabianchi (COP 28), kushiriki kikamilifu katika mkutano huo unaotarajiwa kufanyika Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Novemba 28 hadi Desemba 5, 2023 utakuwa ni adhimu ya kuitangaza Tanzania inavyofanya ufugaji rafiki wa mazingira.

Waziri Jafo alitoa wito kwa CHAMAUTA kulitumia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), kupata uelewa kuhusu kanuni zinazosimamia mazingira ili kuepuka uharibifu.

MWANANCHI UK14

# Maabara mpya kuifunga sekta ya ngozi, viwanda vya nguo nchini

Devotha Kihwelo, Mwananchi
mwananchi@mwananchi.co.tz

Katika mwaka 2022/2023, idadi ya mifugo nchini iliongezeka kutoka ng'ombe milioni 35.3 hadi ng'ombe milioni 36.6, mbuzi kutoka milioni 25.6 hadi milioni 26.6 na kondoo kutoka milioni 8.5 hadi milioni 9.1.

Uwepo wa mifugo mingi ni chanzo cha shughuli mbalimbali za kiuchumi, kuanzia ufugaji wenyewe na uchakataji wa bidhaa za mifugo kama nyama, maziwa, ngozi, mifupa na pembe.

Miongoni mwa mambo yaliyokuwa yanasubiriwa na wafanyabiashara wa sekta ya ngozi ili kukuza biashara zao ni uwepo wa maabara ya kupima ubora wa bidhaa hiyo itokanayo na shughuli za ufugaji.

Kutokana na umuhimu wake Serikali kupitia Shirika la Utafiti wa Viwanda na Maendeleo (TIRDO) iliamua kuanzisha maabara ya ngozi na nguo kwa gharama ya Sh2 bilioni ili kudhibiti ubora wa bidhaa hizo.

Hatua hiyo ilikuwa ni utekelezaji wa ahadi ya muda mrefu ambayo Serikali imekuwa ikitoa kwa wadau wa ngozi nchini kuwa itaanzisha na kuendeleza maabara ya hiyo.

Maabara hiyo ambayo ilianza kufanya kazi mwanzoni kwa Septemba, mwaka huu na ina uwezo wa kupima sampuli zinazowakilishwa ndani ya muda mfupi.

Katibu Mtendaji wa Chama cha Wadau wa Ngozi Tanzania (LAT) Freddy Kabala anasema kuwepo kwa maabara hiyo kutasaidia kuongeza ubora wa bidhaa hiyo muhimu ya utengenezaji wa bidhaa tofauti zikiwemo viatu na pochi.

"Wenye viwanda wanaponunua ngozi huzingatia ubora hivyo kuwepo kwa maabara kutasaidia watu kufanya biashara ya uhakika," anasema.

Anasema maabara hiyo haitasaidia tu wafanyabiashara bali ustawi wa jamii na nchi kwa ujumla kwa kufungua uchumi

**36.6 mil**

**Idadi ya ng'ombe waliopo hapa nchini kwa takwimu za mwaka 2022/2023.**

**Sh2 bil**

**Fedha zilizowekezwa na Shirika la Utafiti wa Viwanda na Maendeleo (Tirdo) kwa ajili ya kuanzisha maabara ya ngozi na nguo.**

kupitia bidhaa za ngozi.

"Kitu ambacho kinafanyika kwa sasa kwa Wizara ya Viwanda na Mifugo wameamua kutoa elimu kwenye utunzaji wa ngozi za wanyama kwa kudhibiti upigaji chapa za moto hivyo kuwapa maelekezo ya sehemu za kuweka alama husika," anasema.

Kabala anasema wafugaji wengi hawaoni manufaa ya ngozi hivyo walikuwa wakizingatia zaidi maziwa na nyama lakini sasa wanajua nguvu ya ngozi katika kuimarisha uchumi wao.

Hata hivyo Kabala anasema maabara hiyo itaongeza kuaminika kwa ngozi ya Tanzania katika soko la kimataifa kwani wanunuzi sasa wanakuwa wanafahamu taarifa za ngozi hiyo tofauti na awali.

Mtafiti kitengo cha ngozi na nguo Tirdo Mhandisi Bosco Mtweve anasema kabla ya kujengwa kwa maabara hiyo wafanyabiashara wa ngozi walikuwa wanaanguka katika biashara zao kutokana na ukosefu wa maabara inayopima ubora wa ngozi.

Mtweve anasema wengine wanaoharibu ngozi ni wachunaji ambao wanakata ngozi bila kufuata utaratibu unaokubalika wa kutunza ngozi katika mazingira mazuri.

"Tumeanza





## ...fifaa vya maabara

UHURU UK 5

# Fursa kwa wavuvi, kuwezeshwa boti

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imetenga fedha za kuwawezesha wavuvi boti za kisasa ambazo zitatolewa katika maeneo yenye shughuli za uvuvi nchini.

Taarifa hiyo ilitolewa Bungeni jijini hapa na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, David Silinde wakati akijibu swali la Mbunge wa Ludewa (CCM), Joseph Kamonga.

Mbunge huyo, alihoji kuwa ni lini elimu ya uvuvi na mikopo ya vifaa vya kisasa, vitatolewa kwa wananchi wa Manda, Ruhuhu, Lweala, Lupingu, Lifuma, Makonde na Lumbila.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Silinde, alisema katika awamu ya kwanza ya mradi wa kuwawezesha wavuvi boti za kisasa, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imetoa jumla ya boti nne za kisasa kwa wavuvi wa Ziwa Nyasa.

> **Katika hatua za awali za upatikanaji wa wanufaika wa mikopo hiyo, wavuvi wa Ludewa...**
>
> Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, David Silinde.

Alifafanua kuwa, kati ya boti hizo, mbili zimetengwa kwa wanufaika wa Halmashauri ya Ludewa ambazo zitakabidhiwa hivi karibuni.

"Katika hatua za awali za upatikanaji wa wanufaika wa mikopo hiyo, wavuvi wa Ludewa, Kata za Manda, Ruhuhu, Lumbila, Lupingu na Ludewa, walipatiwa elimu na mafunzo ya uvuvi endelevu na utaratibu, upatikanaji na urejeshaji wa mikopo yaliyofanyika Oktoba 16 - 25 mwaka jana,"alisema.

Aliongeza; "Katika mwaka huu wa fedha, wizara imetenga fedha za kuwawezesha wavuvi boti za kisasa ambazo zitatolewa katika maeneo yenye shughuli za uvuvi nchini ikiwemo Halmashauri ya Ludewa.

Katika hatua nyingine, Silinde alisisitiza kuwa, katika mwaka huu wa fedha, wizara itaendelea kutoa elimu na mafunzo ya uvuvi endelevu, ujasiriamali katika uvuvi na namna ya kunufaika na fursa za mikopo kutoka taasisi mbalimbali za fedha ikiwemo TADB kwa wananchi wa maeneo ya uvuvi ikiwemo Ludewa.



74>>Bei ya petroli Dar es Salaam iliyotangazwa na EWURA

e ya
Dar

okeza
yo na
bi ya
hadi

Kliniki
a na
wete
zania
atika
a wa

ji la
oto,
gwa
nchi

# RC Songwe awaonya wanaofugia kuku, kuvulia samaki vyandarua

Na MWANDISHI WETU

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Dk. Francis Michael, ameonya matumizi mabaya ya vyandarua yakiwemo kufugia kuku au kuvulia samaki.

Akizungumza mkoani hapa jana, katika uzinduzi wa mpango wa ugawaji wa vyandarua katika shule za msingi, Dk. Micheal alisema vitendo hivyo vinaathiri juhudi za serikali na wadau wa afya katika kupambana na malaria.

Pia, alisema ni utovu wa nidhamu na upotevu wa rasilimali muhimu kwa wananchi kutumia vyandarua kufugia kuku au kuvulia samaki, hivyo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wanaokiuka agizo hilo.

"Mpango wa ugawaji vyandarua kupitia shule za msingi, unalenga kufikisha vyandarua kwa familia zote na kuongeza uelewa kuhusu matumizi sahihi.

"Lengo ni kupambana na malaria, nitoe onyo nikikuta vyandarua hivi vinafugiwa kuku au kuvulia samaki nitachukua hatua kali," alisema.

Alisisitiza dhamira ya serikali ni kuona mkoa huo unaendelea kuwa mfano wa kudhibiti malaria na wananchi wake wanakuwa na afya bora.

Alisema Songwe inajivunia kiwango cha chini cha maambukizi ya malaria ingawa kuna umuhimu wa kudumisha udhibiti huo.

Alisema mpango mkakati uliopo ni kutokomeza malaria, ambapo kipaumbele cha kwanza ni ugawaji wa vyandarua vyenye dawa na elimu ya matumizi sahihi, hususan kwa watoto na wanafunzi waliopo shuleni.

Kwa upande wake Meneja wa Bohari ya Dawa (MSD) Kanda ya Mbeya, Marco Masala, alisema bohari kwa kuwa wao ni wasambazaji wa vyandarua hivyo kwa jamii, watahakikisha lengo linafikiwa.

ZAWADI